TANGAZO LA SERIKALI NA. 24 la tarehe 20/1/2023

SHERIA YA KANDA ZA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE,
(SURA YA 373)

# NOTISI

(*Inatolewa chini ya kifungu cha 3(1)*)

NOTISI YA TAMKO LA KANDA YA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE YA MWAKA 2023

Sura 373

KWA KUWA, kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, kinampa mamlaka Waziri, baada ya kushauriwa na Bodi na kwa kushauriana na mamlaka husika na kwa mapendekezo ya Mamlaka, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali-

(a) kuanzisha au kutangaza eneo lolote la ardhi kuwa Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje; na

(b) kuamua eneo, ukubwa na sifa halisi za mipaka ya Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje;

NA KWA KUWA, Bodi imemshauri Waziri kutangaza eneo la ardhi kuwa Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje na Waziri baada ya kushauriwa, alishauriana na mamlaka husika na mamlaka hizo kuridhia kutangazwa kwa eneo la ardhi lililoainishwa kwenye Jedwali la Notisi hii;

Sura ya 373

HIVYO BASI, katika kutekeleza mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, Mimi, ASHATU K. KIJAJI, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, natangaza eneo lifuatalo kuwa Kanda ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje:

*Tangazo la Serikali Na.24 (Linaendelea.)*

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Tamko la Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje ya Mwaka 2023.

Tamko la Kanda ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje

2. Eneo la ardhi lililoainishwa katika Jedwali la Notisi hii linatangazwa kuwa eneo la Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya nje.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

ENEO LILILOTANGAZWA KUWA KANDA YA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Eneo: | Kata ya Kalangalala iliyopo Wilaya ya Geita ndani ya Mkoa wa Geita |
| | Kiwanja Na: | 257, Kitalu "E" |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | 233.3 Mita za Mraba |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Halmashauri ya Mji wa Geita |
| | Jina la aliyepewa: | GG Refinery Export Processing Zone |

Dodoma,
30 Desemba, 2022

ASHATU K. KIJAJI,
*Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara*